Kama unataka kujifunza zaidi njia ya Mkristo wa kweli anavyopaswa kuishi, basi ni lazima ujifunze Biblia. Ili kukusaidia; Kanise la Christadelphian Bible Mission limechapisha kijitabu kuhusu mafunzo ya Biblia kaitka somo hili muhimu.

Lina itwa Kuishi katika Ukweli. Unaweza kupata nakala kutoka Kanisa la Christadelphian, au kutoka anuani iliyoandikwa katika kijitabu hiki.

CBM Publishing
32 Blenheim Road, Far Cotton
Northampton, England. NN4 8NW

ISBN 1 902059 12 -3
Registered Charity Number: 248979 / 1020558
Company Number: 2796412
Telephone +44 (0) 1604 765068
Facsimile +44 (0) 1604 463578
Email: CarlHinton@hotmail.com
Web: http:\\go.to\Carl_Hinton

9781902059129

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN 37-40
Correspondence Course Lessons 37-40

Tena:

1 902059 00 - X	Matayarisho ya Ubatizo
1 902059 01 - 8	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 1-4
1 902059 02 - 6	Ukimwi
1 902059 03 - 4	Mshitaki Wenu Ibilisi
1 902059 04 - 2	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 5-8
1 902059 05 - 0	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 9-11
1 902059 06 - 9	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 12-15
1 902059 07 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 16-19
1 902059 08 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 20-23
1 902059 09 - 3	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 24-27
1 902059 10 - 7	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 28-31
1 902059 11 - 5	Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 32-36
1 902059 12 - 3	**Masomo ya Biblia kwa njia ya posta ya Wakristadelphian 37-40**
1 902059 13 - 1	Ufunuo mlango wa kwanza - Maelezo ya maneno ya mstari kwa mstari

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na 37.

KUSOMA BIBLIA KILA SIKU
Soma: Zaburi 119:89-112

Biblia ni kama kisima kirefu cha maji safi - kisima kilicho kwenda chini mno ambacho kamwe huwezi kufika kwenye kitako chake. Kamwe hutaweza kufika katika wakati utakapo jiona kuwa unaijua yote, ya kuwa huna haja tena ya kusoma Neno la Mungu.

Tazama jinsi watu wanavyo lipokea Neno la Mungu.

WABEREA KULE UYUNANI . . .	PAULO ALIWAANDIKIA WATHESALONIKE:
"... walilipokea neno kwa utayri wa moyo wote, na waliyachunguza Maandiko kila siku, ikiwa mambo hayo yalikuwa hivyo, na kwa sababu hiyo wengi wao waliamini" (Matendo 17:1 1 ,12)	"Wakati ninyi mlipo lipokea neno la Mungu mlilo lisikia toka kwetu, ninyi hamkulipokea kama ni neno la kutoka kwa wanadamu, bali kama kweli, neno la Mungu" (1 Wathesalonike 2:13)

kusome kwa makini kitabu hiki!

Mungu anazungumza nasi katika kitabu ! Kinatupa tumaini la uzima kwa njia ya injili.

Biblia na Yesu

Kwa kweli, Yesu, alikuwa na Agano la Kale tu. Lakini namna alivyo lijua vema! Katika kila shida na tatizo, moja kwa moja alikwenda kwenye Neno la Mungu ili kupata jibu. Tazama mifano hii:

1. Wakati Mafarisayo walipo muuliza ikiziwa ilikuwa vema mitu kumpa talaka (kumuacha) mkewe, Yesu alikwenda moja kwa moja kwenye masimulizi ya Adamu na Eva katika kitabu cha Mwanzo. Aliwaambia: "Tangu mwanzo wa uumbaji Mungu aliwaumba mwanaume na mwanamke." Unaweza kusoma habari yote ya jibu lake katika Marko 10:5-12.
2. Wakati Yesu alipokuwa peke yake jangwani, majaribu yalimjia ili aende katika njia iliyo nyepesi kwake, badala ya kwenda njia ya Mungu. Aliyashinda mawazo haya mabaya kwa kuyajibu na maneno ya kutoka kitabu cha Kumbukumbu la Torati, na kila muda alisema: "Imeandikwa . . . "
3. Wakati askari walipokuja kumkamata, Yesu alijua kifo kitafuata. Alikwenda bila kushindana, kwa sababu alisema, "inapasa Maandiko yatimie" (Marko 14:49), na Maandiko yalitabiri kifo chake. Katika maisha yake yote, Yesu alikuwa anatimiza yaliyokuwa yameandikwa kuhusu yeye kwenye Agano la Kale.

17. Kwa nini Agano la Kale ni la Muhimu?
18. Kwa nini ni muhimu kwa waamini walio batizwa kwa kawaida kushika utumishi wa kuumega mkate na kunywa divai?
19. Kwa nini Wakristo tu washirikiane (washiriki mkate na divai) pamoja na Wakristo wengine wa Kweli?
20. Jinsi gani dhambi zaweza kusamehewa baada ya ubatizo?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

Kukua katika kumjua Yesu

Petro anatuambia "tukue katika neema, na katika kumjua Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo" (2 Petro 3:18). Tunaweza kupata kumjua Yesu kwa kusoma kuhusu yeye, na katika kila moja ya injili nne zinatuambia habari ya kile Yesu alicho sema na kufanya, na jinsi alivyo toa uhai wake kwa ajili yetu.

Vitabu vingine vya Agano Jipya vinatusaidiakufahamu kuhusu yote ambayo Yesu alifanya kwa ajili yetu kwa kufa msalabani, na jinsi ya kuishi katika maisha mapya katika Kristo.

Lakini haiwezekani kufahamu mambo haya pasipo kusoma Agano la Kale pia. Mstari wa kwanza wa Agano Jipya (Mathayo 1:1) unasema kuhusu "Yesu Kristo, Mwana wa Daudi, mwana wa Abrahamu". Yatupasa kwenda kwenye Agano la Kale ili kupata watu hawa walikuwa ni akina nani, na kwanini Yesu ameitwa ni mwana wao.

Yesu alisoma Agano !a Kale; nasi yatupasa pia

Tunahitajika kusoma kila siku

Mitume Paulo anatuambia jinsi ilivyo ni muhimu kusoma Maandiko katika maisha yetu:

> "Maandiko yote yametolewa kwa uongozi wa Mungu na **yafaa** kwa mafundisho, kwa kuonya, kwa kuadibisha na kufundisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilika vema kwa kazi zote njema."
> (2 Timotheo 3:16, 17).

Mungu anatupa chakula kinacho hitajika katika mwili siku kwa siku. Yesu anawakumbusi wafuasi wake hili wakati alipo waambia:

> *"Waangalieni ndege wa angani ya kwamba hawapandi, wala hawakusanyi ghalani; lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha hao. Je ninyi sio bora kuliko hao?"(Mathayo 6:26).*

Katika njia hiyo hiyo, maisha yetu mapya katika Kristo yatakuwa iwapo yatalishwa na chakula kinacho hitajika ni Neno la Mungu.

Itakuwa ni hatari kama tutashinda bila chakula kwa wiki, na kisha kufikiria kufa chakula chote cha wiki kwa mara moja. Kwa njia hiyo hiyo, tunahitaji kuilisha akili yetu kila siku na Neno la Mungu. Kama tukifanya hivyo, ufahamu wetu utajengeka katika njia zake, na tutakua katika neema na maarifa.

Kusoma Maandiko yote

Sehemu zingine za Biblia, kama Zaburi na masimulizi ya injili, zina furahisha kusoma. Lakini sehemu zingine zinasimulia habari za ukatili wa ukaidi na vita, na hatupendezewi kuzisoma mno. Sura zingine zina habari ndefu za watu na sehemu, nasi tunaweza kushangaa kwa nini zipo hapo. Lakini, kama tulivyo soma 2 Timotheo 3:16, Maandiko yote yafaa. Wanaume na wanawake wana mahitaji mengi tofauti, tabia, mambo na namna ya kujipatia maarifa na Maandiko yana watosheleza wote.

Kutoka mstari wa kwanza wa kitabu cha Mwanzo hadi kitabu cha mwisho cha Ufunuo, Biblia ni pumzi ya Neno la Mungu. Ikiwa tungeambiwa kuchagua wenyewe, tungesoma sehemu zilizo na mambo ya kufurahisha. Tusinge kuja kuelewa mafundisho ya Mungu yaliyo ya muhimu zaidi katika Biblia: uovu ulio ndani ya mwanadamu, utakatifu mkuu wa Mungu na kicho cha Bwana na utii anao utaka toka kwetu.

Haja ya kuwa na mpango

Ili kuhakikisha kuwa tunasoma Maandiko, twahitajika kupanga usomaji wetu.
Wakati umefika sasa wa kuanza kusoma Biblia kwa mpango unao itwa katika kitabu Kidogo Bible Planner (yaani kusoma Biblia kwa mpango). Njia hii itakuchukua katika Biblia yote kwa njia ya kupendeza, na muhutasari katika Kitabu Kidogo cha kuangalia maelezo mafupi kitakusaidi kuelewa kusoma.

Na wakati ukiisha maliza kazi kwa kupitia mpango huu - kisha kinafuatia nini?

Ndipo utakuwa tayari kusoma kila siku toka kwenye kitabu kidogo kingine kinacho itwa MWENZI WA BIBLIA, ambacho kinaweza kutumwa kwako pamoja na masomo. Utaratibu huu wa kusoma utakuchukua katika Agano la Kale mara moja, na Agano Jipya mara ya pili kila mwaka mmoja, na utaona hakika unaanza kuijua Biblia yako.

Kumbuka, pia, kuwa wa-Christadelphian ulimwenguni pote huwa wanatumia mpango huu; wote wanatafuta kukua katika ufahamu wa Neno la Mungu, hivyo haupo peke yako katika kusoma kwako.

SEHEMU ZINGINE ZA KUFAA

Namna ya kusoma

Ni wazo zuri wakati unasoma Biblia yako kila siku, kusoma sura nzima kwanza ni kutafuta inasema nini. Baada ya kusoma, fumba macho yako na useme mwenyewe, "Umesoma nini". Wakati mwingine utaweza kukumbuka vema kabisa; wakati mwingine utaona shida. Basi unahitajika kusoma tena sura yote.

3. Nafsi maana yake nini? _____
4. Ahadi gani ilitolewa na malaika wakati Yesu alipo paa kuelekea Mbinguni? _____
5. Ubatizo ni kitu gani? _____
6. Ibilisi ni nani? _____
7. Mapepo ni vitu gani? _____
8. Roho Mtakatifu ni nani? _____

FUNGU D Jibu fupi: KWA NINI?

1. Kwa nini Mungu aliuumba ulimwengu? _____
2. Kwa nini Mungu aliugharikisha ulimwengu? _____
3. Kwa nini Abrahamu alibarikiwa na Mungu? _____
4. Kwa nini tunahitaji kusoma Biblia? _____
5. Kwa nini Wayahudi walitwaliwa utumwani? _____
6. Kwa nini Mungu aliruhusu Yesu afe msalabani? _____
7. Kwa nini Yesu alifufuliwa toka wafu? _____
8. Kwa nini tunafanya dhambi? _____
9. Kwa nini zawadi za Roho Mtakatifu zilitolewa? _____
10. Kwa nini Wakristo yawapasa kuoana na Wakristo? _____

FUNGU E Ndiyo au Hapana?

1. Je, Yesu alikuwepo wakati wa Agano la Kale? _____
2. Wakristo wajihusishe na siasa? _____
3. Wakristo waipiganie nchi yao? _____
4. Je, "shetani" anaweza kutumika kuwataja watu wema. _____
5. Je Ufalme wa Mungu ulikuwepo zamani za wakati wa Agano la Kale? _____
6. Je zawadi za Roho Mtakatifu (kama kunena kwa lugha) zipo leo? _____
7. Yesu na Mungu wapo sawa? _____
8. Je Wakristo waitunze siku ya saba (Sabato) kwa ajili ya kuabudu? _____
9. Je, "takatifu" maana yake tenga? _____
10. Wakristo wafanye tendo la ndoa kabla ya kuoana? _____

FUNGU F Maswali yenye majibu marefu (tafadhali jibu kwenye karatasi ingine)

1. Kwa nini waamini wa kweli wabatizwe?
2. Panatokea nini mara tukifa?
3. Kutatokea nini kwenye hukumu?
4. Kwa nini Yesu ilibidi afe?
5. Kwa nini Biblia inatumia shauri la ibilisi?
6. Ufalme ujao wa Mungu utafananaje?

KARATASI YA SWALI-MWISHO

Testi ya mwisho inauliza kuhusu kozi nzima. Tafadhali jibu mafungu A, B, C, D na E kwenye nafasi za maswali ambazo zipo wazi katika karatasi. Tafadhali jibu fungu F kwenye karatasi nyingine na halafu tuma majibu yako kwa mfunzi wako. Usisahau kuandika jina lako.

FUNGU A Majibu neno 1: NINANI?

1. Ninani aliumba ulimwengu _____
2. Ninani aliumbwa kutoka mavumbini? _____
3. Ninani aliahidiwa kuwa atairithi nchi ya Kanaani (Israeli) _____
4. Ninani alipokea maelezo ya kujenga hema ya kukutania? _____
5. Ninani aliahidiwa kuwa atakuwa na "mwana" wa kutawala kiti chake milele? _____
6. Huyu "mwana" ninani katika swali lilopita? _____
7. Yesu alimwita ni nani "Shetani" ? _____
8. Yesu alimfufua nani toka wafu? _____
9. Ni nani atahukumu ulimwengu? _____
10. Ni nani aliwaongoza watu kuandika Biblia? _____

FUNGU B Majibu neno 1: WAPI?

1. Abrahamu alikuwa anaishi wapi hapo kwanza? _____
2. Ni wapi alikofanywa Yusufu kuwa mtawala? _____
3. Ni wapi aliko zipokea sheria Musa alizo wapa watu wake Mungu? _____
4. Kiti cha enzi cha Daudi kilikuwa wapi? _____
5. Ni wapi aliko kuwa utumwani Danieli? _____
6. Mlima Sayuni upo wapi? _____
7. Yesu alizaliwa wapi? _____
8. Yesu alibatizwa wapi? _____
9. Kuzimu ni wapi? _____
10. Kitovu cha Ufalme wa Mungu kitakuwa wapi? _____

FUNGU C Jibu fupi: NINI?

1. Ni taifa gani ambalo Mungu alifanya kuwa ni taifa la watu wake? _____
2. Injili maana yake nini? _____
3. Neema nini? _____
4. Kurudi kwa Wayahudi kunanyesha nini? Katika nchi yao? _____

Msaada mwingine wa kusoma Biblia

Ikiwa Biblia yako haina ramani au hataji mistari kwa pembeni, au imeandikwa namna tofauti, hakuna tabu-bado una Neno la Mungu. Ingawa hivyo, kwa wale walio na msaada wa ziada katika Biblia zao, maelezo mafupi yafuatayo yatakusaidia kwa kuyatumia:

a) Vifungu vya maneno vinavyo tajwa pembeni

Biblia zingine zinavyo, Biblia ikiwa navyo inasaidia sana. Unaweza kupata herufi ndogo au namba ya neno: na herufi au namba inaweza kupatikana pambizoni. Hapa itakupa sura na mstari uliounganishwa na pale ulipo soma. Utazame. Utapata msaada wa kuilewa sura unayo isoma.

b) Sura na mistari

Sio kama kitabu kingine chochote, Biblia imegawanyika katika sura na mistari vile vile. Sura na mistari iliwekwa miaka mia nyingi baada ya Biblia kukamilika. Hakika inasaidia kuhusu kuitafuta njia yako.

Lakini sio siku zote inasaidia. Wakati mwingine inagawanya habari katika sehemu mbili, kama katika habari ya Yesu kubadilika sura katika Mathayo 16 na 17. Mstari wa mwisho katika sura ya 16 unasomeka, "Pana watu wengine wasimamao hapa, ambao hawata onja mauti, hata wamuone mwana wa Adamu akija katika Ufalme wake."

Yesu anazungumzia kuhusu maono ya Ufalme ambayo yalitolewa kwa watatu wa wanafunzi wake, Petro, Yakobo na Yohana ndugu yake. Sura ya 17 inaanza, "Na baada ya siku sita Yesu aliwatwaa Petro, Yakobo na ndugu yake Yohana, na akawaleta kwenye mlima mrefu faraghani". Basi wakati unaanza kusoma Mathayo 17, unatakiwa kuangalia nyuma kwenye mstari wa mwisho wa sura ya 16 kwanza.

Siku zote ni shauri jema kuangalia "fungu !a maneno" (au mistari inayozunguka) Ya sura ambayo unaisoma, ili kuona kipi kinakuja kabla na kinacho fuata.

c) Tumia ramani zako

Biblia zingine zina ramani upande wa nyuma. Unapo soma kuhusu tukio lililo tokea mahali fulani, itafute sehemu hiyo katika ramani yako. Kama ukifanya hivi kila mara ukitafuta mji, mto, mlima au ziwa lililo tajwa, utakuja kuijua nchi ya Israeli kidogo vizuri. Vile vile, unaweza kuielewa habari vizuri.

Kwa mfano ukuisoma Luka 2 (Hatua 1, siku ya 3 katika planna yako) utauona mji wa Nazareti, Bethelehemu na Yerusalemu ambayo miji hii yote inakuja katika habari. Sasa tazama ramani, na utaona kwamba ni mwendo kutoka Nazareti hadi Bethelehemu, lakini Bethelehemu na Yerusalemu imekaribiana.

Soma Biblia yako kwa kuomba

Popote utakapo kaa ili kuisoma Biblia yako, muombe Mungu ili akusaidie uielewe Biblia ambayo ni Neno la Mungu. Kuna mstari katika Zaburi ya 119 (mstari 18) ambao ni sala. Unasema:

> *"Unifumbue macho yangu ili niyaone maajabu ya kutoka katika sheria yako".*

lli kuelewa tunahitaji msaada wa Mungu, na kila siku yupo tayari kutoa - basi usisahau kuomba!

Kusikia na kufanya

Mungu atatufundisha katika neno lake. Lakini kusoma haitoshi. Yakobo anatuambia yatupasa kuwa "watendaji wa neno, na sio wasikiaji tu" (Yakobo 1:22). Yesu amewataja wengine wanao mwita "Bwana, Bwana", ambao hawakufanya yale aliyowataka kufanya. Soma Mathayo 25: 31-46.

Sasa tafuta Mathayo 7, na halafu soma habari katika mistari 24-29 kuhusu watu wawili walio jenga nyumba za aina moja, Mtu anaye sikia anayo yasema Yesu, **na kutekeleza** anayo sema, ni sawa na mtu mwenye busara aliye jenga nyumba yake kwenye mwamba.

Njoo kwenye Biblia na moyo wa unyenyekevu

Mungu amesema:

> *Mtu huyu ndiye nitakaye mwangali aliye mnyonge na mnyenyekevu wa roho anaye tetemeka kwa maneno yangu" (Isaya 66:2)*

Mungu atamfundisha mtu aliye na unyenyekevu wa moyo, aliye tayari kujifunza: Hata kuwa na kitu cha kufanya na mtu anayesema anajua yote !

Muhutasari

Soma BIBLIA ...

... kila siku. Hakika kama utasoma Biblia itakuwa ni jambo zuri na ushauri ni kuwa hakikisha unasoma Agano 1a Kale na Jipya.
... pamoja na moyo ulio wazi, iruhusu ikufundishe **wewe.**
... kwa uangalifu. Utafakari kila mstari na hakikisha unauelewa.
... kwa sala. Muombe Mungu akusaidie i1i ufahamu unayo soma.
... Kwa unyenyekevu wa moyo, jaribu kutafuta jinsi Mungu anavyo taka namna ya wewe kuishi,

7. Kwa nini Agano la Kale ni la Muhimu?
8. Kwa nini ni muhimu kwa waamini walio batizwa kwa kawaida kushika utumishi wa kuumega mkate na kunywa divai?
9. Kwa nini Wakristo tu washirikiane (washiriki mkate na divai) pamoja na Wakristo wengine wa Kweli?
10. Jinsi gani dhambi zaweza kusamehewa baada ya ubatizo?

Tuma majibu yako kwa:

Jina lako ni:

Christadelphian Bible Mission Box CBM, 404 Shaftmoor Lane,
Birmingham B28 8SZ, England

5. Nafsi maana yake nini? _____
6. Ahadi gani ilitolewa na malaika wakati Yesu alipo paa kuelekea Mbinguni? _____
7. Ubatizo ni kitu gani? _____
8. Ibilisi ni nani? _____
9. Mapepo ni vitu gani? _____
10. Roho Mtakatifu ni nani? _____

FUNGU D Jibu fupi: KWA NINI?

1. Kwa nini Mungu aliuumba ulimwengu? _____
2. Kwa nini Mungu aliugharikisha ulimwengu? _____
3. Kwa nini Abrahamu alibarikiwa na Mungu? _____
4. Kwa nini tunahitaji kusoma Biblia? _____
5. Kwa nini Wayahudi walitwaliwa utumwani? _____
6. Kwa nini Mungu aliruhusu Yesu afe msalabani? _____
7. Kwa nini Yesu alifufuliwa toka wafu? _____
8. Kwa nini tunafanya dhambi? _____
9. Kwa nini zawadi za Roho Mtakatifu zilitolewa? _____
10. Kwa nini Wakristo yawapasa kuoana na Wakristo? _____

FUNGU E Ndiyo au Hapana?

1. Je, Yesu alikuwepo wakati wa Agano la Kale? _____
2. Wakristo wajihusishe na siasa? _____
3. Wakristo waipiganie nchi yao? _____
4. Je, "shetani" anaweza kutumika kuwataja watu wema. _____
5. Je Ufalme wa Mungu ulikuwepo zamani za wakati wa Agano la Kale? _____
6. Je zawadi za Roho Mtakatifu (kama kunena kwa lugha) zipo leo? _____
7. Yesu na Mungu wapo sawa? _____
8. Je Wakristo waitunze siku ya saba (Sabato) kwa ajili ya kuabudu? _____
9. Je, "takatifu" maana yake tenga? _____
10. Wakristo wafanye tendo la ndoa kabla ya kuoana? _____

FUNGU F Maswali yenye majibu marefu (tafadhali jibu kwenye karatasi ingine)

1. Kwa nini waamini wa kweli wabatizwe?
2. Panatokea nini mara tukifa?
3. Kutatokea nini kwenye hukumu?
4. Kwa nini Yesu ilibidi afe?
5. Kwa nini Biblia inatumia shauri la ibilisi?
6. Ufalme ujao wa Mungu utafananaje?

Sura za kusoma: Zaburi 19; 119:1-40; Marko 8:34-38
Mstari wa kujifunza: Zaburi 119: 33,34

"Unifundishe Ee Bwana njia ya amri zao; nami nitazishika hata mwisho. Unipe ufahamu nami nitaishika sheria yako; naam, nitaitii kwa moyo wangu wote".

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na38.

USHIRIKA PAMOJA NA WALE WENYE IMANI MOJA
Soma: 1 Wakorintho 3

Hapo Mungu alipo muumba mwanadamu, ilikuwa ni kilele cha kazi yake ya uumbaji. Mtu aliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwanzo 1:27), aliumbwa ili kwamba awe kama Mungu, pamoja na akili iliyo kua ya mema na mabaya.

Lakini hata hivyo, kulikuwa na kitu kingine kilicho kosekana: mtu alikuwa peke yake, na katika rehema zake Mungu aliweza kutambua kwamba Adamu alihitaji wa kufuatana naye. Basi, alimuumba mwanamke pia, akitoa sababu:

"Si vema mtu huyo awe peke yake" (Mwanzo 2:18).

Ushirika nini?

Adama na Eva waliumbwa kwa ajili ya kila mmoja na ilikuwa na maana wasaidiane (2:18). Wakati Eva alipo letwa kwake, Adamu alisema, "Sasa huu ni mfupa katika mifupa yangu, na mwili katika mwili wangu" (Mwanzo 2:23), na mwandishi aliye ongozwa na Mungu anaongezea kwamba mwanaume na mke watafuatana (au wataungana) pamoja (Mwanzo 2:24).

Huu ulikuwa ni ushirika - wakishirikiana katika yote ambayo Mungu aliwapa, kila mmoja akimfurahia mwenzake, na kushukuru pamoja katika baraka zote za Mungu. Hapo Bwana Mungu alipokuja kwenye bustani wakati wa jua kupoa, urafiki ulikuzwa - wakawa wamoja na Mungu. Katika bustani ya Edeni, mwanaume, mwanamke na Mungu walikuwa katika upatano kamili.

Lakini mapatano hayakudumu. Hapo dhambi ilipo ingia ulimwenguni, ushirika ulivunjika. Mungu ni mtakatifu, haikubali dhambi, wala wenye dhambi hawawezi kuwapo mbele ya utakatifu wake. Kukawa na mgawanyiko pale ulipo umbwa mara sheria ya Mungu lipovunjwa. (soma Mwanzo 3 tena). Hapo Mungu alipokuja bustanini kutembea siku ile, Adamu na Eva walijua wapo uchi (3:7).

Ushirika ulivunjika. Uhusiano wao wanadamu ulibadilika (Adamu alimlaumu Eva kwa kile kilicho tokea), na mshikamano wao wa karibu ulikoma na Mungu. Sasa waliweza kuja mbele zake tu kwa njia aliyo itoa. Ilibidi waiache Bustani, na maisha yakawa ni kazi ngumu.

Lakini ushirika kuupata umebaki ni ule ule, hata kama hali ya mambo tunayo yatafuta sasa yapo tofauti sana. Tunapo shirikiana sisi kwa sisi, ina maana kwamba tunaweza kushiriki baraka za Mungu na wengine wanao amini kama sisi, na kuwa na tumaini la wokovu mmoja. Ushirika unaweza kuwepo hata kati ya watu hawajawahi kukutana, kwa mfano, kwa sababu wamekuwa wakiandikiana na wamekuwa wanashirikiana maisha yao namna hhiyo. Ushirikiano unaweza kuwepo pamoja na watu wanao abudu pamoja, na pamoja na watu wanao ishi na kufanya kazi pamoja - wamegawiwa kuwa na imani moja ya Kikristo.

Ulimwenguni pote, wanaume na wanawake wanashirikiana pamoja wanapokuwa wanahusika katika familia ya Mungu. Ushirika sio kitu kimoja kama kuendelea vema na mtu mwingine - ni uhusiano wa kiroho ambao unategemea juu ya kushirikiana imani moja kwa Mungu.

> Ushirika maana yake kushirikiana. Ushirikiana wa Biblia maana yake ni kushiriki imani, matumaini, na kuabudu pamoja na ndugu-waamini

Roho na Kweli

Moja ya safari zake nchini Israeli, Yesu alikwenda kupitia Samaria - sehemu ya nchi ambayo ilikaliwa na watu waliokuwa hawapendwi na Wayahudi. Yesu alikuwa hana chuki kama hizi, na alipo pata nafasi ya kukaa karibu na kisima, akazungumza na mwanamke wa. Samaria. Muda si mrefu mwanamke akagundua kuwa Yesu alikuwa sio Myahudi wa kawaida, na mwanamke alipo muuliza Yesu alifikiria ni eneo lipi ni takatifu zaidi-moja kwenye mlima Gerizimu karibu na pale walipokuwa wanafanyia mazungumzo, au moja lililo Yerusalemu Yesu alimpa jibu ambalo alikuta linamshangaza. Alimwambia sio mlima ulio wa muhimu, kisha aliongeza:

> *"Saa inakuja, na sasa ipo, ambayo waabuo halisis watamuabudu Baba katika roho na kweli: kwa maana Baba awatafuta watu kama hao ili wamwabudu" (Yo.4:23).*

Karibu miaka 40 baada ya mazungumzo yale, sehemu zote mbili Yerusalemu na mlima Gerizimu palikuwa hakuna mahali palipo patikana pa kufanyia ibada. Warumi waliisafisha nchi ya Israeli katika mwaka 70 BK na kuharibu maeneo ya kidini. Wale wayahudi walio pona matokeo ya vita, na wale ambao hawakuponyoka, walitwaliwa utumwani na waliuzwa kama watumwa. Hivyo ikiwa dini yao ilitegemea juu ya mahekalu na maeneo matakatifu, ilibidi wayaache. Yesu alisema kwamba waabudu wa kweli hawana haja na maeneo na majumba; badala yake wawe na imani, unyoofu, na kweli.

"Roho na kweli" iliyo hapo juu, ni muunganiko ulio wa muhimu sana. Watu wengine wame dai kuwa wanayo, au wanaongozwa na roho. Lakini ukizungumza nao, punde utatambua kwamba hawajui inacho fundisha Biblia. Labda wanaamini kwenda mbinguni wakifa, wakati Biblia inafundisha kwamba tumaini la kweli la Mkristo ni kuwekwa Ufalme wa Mungu duniani. Au wana amini kwamba Yesu ni sehemu ya tatu kitaki mungu-Mmoja, ambapo Biblia inafundisha kwamba ni Mwana wa Mungu, aliye zaliwa toka kwa Bikira Mariamu, kwa uweza, au roho wa Mungu. Watu wanao dai kuwa wanaye roho, na wamepungukiwa na kweli katika Biblia, inabidi kuwa wana kosa.

KARATASI YA SWALI-MWISHO

Testi ya mwisho inauliza kuhusu kozi nzima. Tafadhali jibu mafungu A, B, C, D na E kwenye nafasi za maswali ambazo zipo wazi katika karatasi. Tafadhali jibu fungu F kwenye karatasi nyingine na halafu tuma majibu yako kwa mfunzi wako. Usisahau kuandika jina lako.

FUNGU A Majibu neno 1: NINANI?

1. Ninani aliumba ulimwengu _____
2. Ninani aliumbwa kutoka mavumbini? _____
3. Ninani aliahidiwa kuwa atairithi nchi ya Kanaani (Israeli) _____
4. Ninani alipokea maelezo ya kujenga hema ya kukutania? _____
5. Ninani aliahidiwa kuwa atakuwa na "mwana" wa kutawala kiti chake milele? _____
6. Huyu "mwana" ninani katika swali lilopita? _____
7. Yesu alimwita ni nani "Shetani" ? _____
8. Yesu alimfufua nani toka wafu? _____
9. Ni nani atahukumu ulimwengu? _____
10. Ni nani aliwaongoza watu kuandika Biblia? _____

FUNGU B Majibu neno 1: WAPI?

1. Abrahamu alikuwa anaishi wapi hapo kwanza? _____
2. Ni wapi alikofanywa Yusufu kuwa mtawala? _____
3. Ni wapi aliko zipokea sheria Musa alizo wapa watu wake Mungu? _____
4. Kiti cha enzi cha Daudi kilikuwa wapi? _____
5. Ni wapi aliko kuwa utumwani Danieli? _____
6. Mlima Sayuni upo wapi? _____
7. Yesu alizaliwa wapi? _____
8. Yesu alibatizwa wapi? _____
9. Kuzimu ni wapi? _____
10. Kitovu cha Ufalme wa Mungu kitakuwa wapi? _____

FUNGU C Jibu fupi: NINI?

1. Ni taifa gani ambalo Mungu alifanya kuwa ni taifa la watu wake? _____
2. Injili maana yake nini? _____
3. Neema nini? _____
4. Kurudi kwa Wayahudi kunanyesha nini? Katika nchi yao? _____

"Kama unaamua kubatizwa, itakuwa ni tukio la muhimu zaidi katika maisha yako. Kuwa m-Christadelphian ni kuzaliwa katika familia ya Yesu Kristo, pamoja na ndugu wa kiume na wa kike ulimwenguni pote walio na imani moja na kushiriki undugu wa kweli pamoja nawe."

Hatua ya pili ni rahisi

Mwandikie mfunzi wako, pamoja na kukamilisha kujaza cheti ambacho huja na somo hili.

Kinacho fuata ni kwamba waabudu wa kweli hawata kuwa na mawazo sana ya kuingia mioyoni kuwa na makanisa makubwa, au mahali pa kufanyia ibada, au zuwa na kundi kubwa la washirika wenye shauku. Kanisa la kweli halihusu majengo bali watu; na haidhuru wapo wangapi. Kitu cha muhimu wanacho amini, na jinsi wanavyo mwabudu Mungu. Ni vema kuwa na roho sahihi katika ibada, na vile vile ni muhimu kuamini mambo yaliyo ya kweli na kufanya yaliyo sawa na Mungu.

Mjitenge

Agano Jipya lina agiza wafuasi wa Yesu Kristo waishi kwa kujitenga na ulimwengu. Hii haina maana kuacha ulimwengu - isingewezekana - bali waishi kwa utofauti na ulimwengu toka kwenye njia zake za uasi. Abrahamu alikaa na Wakanani, lakini alijitenga nao. Alielezwa kama ni "mgeni na mpitaji" (Waebrania 11:13), kwa maana alikuwa na matumaini yake na imani aliyo iweka juu ya Mungu na ahadi zake. Katika njia ile ile, Yesu aliwaombea wafuasi wake kwamba walindwe na Mungu kutokana na ulimwengu muovu, aliongeza:

> *"Wao sio wa ulimwengu, kama nisivyo wa ulimwengu. Uwatakase na ile kweli: neno lako ndilo kweli. Kama ulivyo nituma ulimwenguni, nami vivyo nawatuma ulimwenguni" (Yohana 17:16-18).*

Yesu na wafuasi wake waliuangalia ulimwengu (ona 1 Yohana 2:16) kama mahali pabaya na penye uovu. Ulimwengu umejaa watu ambao hawana haja na mambo ya Mungu, na ambao wanayafanya maisha yawe magumu kwa Wakristo wa kweli kutenda kama Mungu anavyo amuru.

Tambua kwamba kwa usawa huu unaweza kuwahusu wenye dini na wasio na dini. Wote wanao ipinga kweli kuhusu Mungu wanapasiwa kuwaongoza waamini wa kweli kupotoka kwa Mungu.

Makao ya Mungu.

Wakati mwingine wa-Christadelphian wameulizwa "Kanisa lenu lipo wapi?", na watu wanategemea kuona jengo zuri ambalo litawafurahisha na kuwathibitisha kwamba kweli hili ni kanisa la Mungu. Ni vigumu watu kama hawa kukubali kwamba Mungu anawataka watu zaidi ya majengo, na hii ilikuwa ni kweli katika siku za Yesu na mitume pia. Kulikuwa na majengo mazuri ambayo watu wengine wakati ule walikwenda kuabudu - hasa kweli hekalu lililokuwa Yerusalemu ambalo lilichukua miaka 40 kulijenga na kuliremba. Bali Yesu alisema hekalu lilikuwa ni pango la wanyan'ganyi wezi; aliwaambia wafuasi wake wamfuate, wasikae pamoja na makuhani.

Hata siku moja Yesu hakujenga jengo la kanisa. Chakula chake cha mwisho alikula pamoja na wafuasi wake katika chumba cha juu Yerusalemu, na kule mitume walikutana wakati fulani baadaye kwa ajili ya ibada (Matendo 1:13; 12:12). Utumishi wa mitume katika kanisa la kwanza ulifanyika nyumbani (angalia Wakolosai 4:15) au kwenye vyumba vya kupanga (Matendo 28:23-31). Kwa maana walifahamu ukweli ulio wa muhimu kuwa wao ndiyo walikuwa makao ya Mungu - Mungu alitaka kuishi ndani yao na pamoja nao kila siku ya maisha yao.

Mtume Paulo anaweza kuwa alikuwa anazungumzia jengo hapo alipo waambia Wakorintho waamini kwamba kazi yake Korintho, ambako alitutumia miezi 18, ilisababisha kuweka msingi (1 Wakorintho 3:10). Alichokuwa anamaanisha, aliweka msingi wa Yesu Kristo kwa kuwafundisha kweli kuhusu Mwana wa Mungu, aliye kufa kwa ajili yao na alifufuliwa na Mungu kwa uzima wa milele. Sasa, alisema Paulo, ilikuwa wajenge juu ya msingi huo kwa jinsi walivyo ishi na kuamini (3:12-15), ndipo aliongezea:

> *"Hamjui ya kwamba ninyi ni hekalu la Mungu, na ya kwamba Roho wa Mungu anakaa ndani yenu?" (mstari 16, pia angalia Waefeso 2:19-22).*

Kuumega Mkate

Mkate na divai ni kikumbusho cha mwili (mkate) na damu (divai) ya Yesu ambayo ilitolewa na kumwagwa kwa ajili ya dhambi zetu msalabani.

Hakuna zitu cha muujiza au cha kutatiza kuhusu hivi vitu; kwa mfano, mkate haubadikikama watu wengine wanao amini vibaya-katika mwili halisi wa Bwana Yesu. Vitu hivyo vinawakumbusha kazi kubwa aliyo ifanya Yesu kwa niaba yao, na ni wamini walio batizwa **pekee** ndiyo wanaweza kushiriki huduma hii ya kukumbuka. Kama Yesu alivyo sema kwa wanafunzi wake,

> *"Fanyeni hivi kwa kunikumbuka" (Luka 22:19).*

Kuumega mkate ni kiini cha ushirika wa Mkristo wa kweli. Waamini wanafanya kila jitihada ili kuhakikisha kuwa wanakutana kila wiki pamoja, wanapoweza, kumkumbuka Bwana wao na kazi kubwa yake ya wokovu. Wanahitaji kukutana mara kwa mara ili waweze kukua pamoja katika upendo, na katika kweli. Kama mtume aliposema:

> *"Tuangaliane sisi kwa sisi na kuhimizana katika upendo na kazi nzuri; wala tusiache kukusanyika pamoja, kama ilivyo desturi ya wengine: lakini tuonyane: na tuzidi kufanya hivyo, kama mnavyo ona siku ile inakaribia" (Waebrania 10:24,25).*

Mapendekezo kadhaa ya kukusaidia

1. Tafadhali rudi nyuma kupitia Masomo toka la 1 hadi 39, kwa kuweka alama ya jambo gumu lolote, na uonyeshe mambo uliyo nukuu ya muhimu katika Biblia yako.
2. Andika na umweleze Mfunzi wako namna unavyo ona yale ulio jifunza kutoka Biblia. Masomo umeyafurahia? Kulikuwa na mambo yaliyo kutatiza? Je unahitaji maelezo zaidi ya masomo mengine?
3. Umekuwa ukitumia kitabu kidogo kinacho itwa Mpango wa Kusoma BIBLIA kwa ajili ya kusoma Biblia kila siku na umepokea kitabu chetu kingine kinacho itwa MWENZI WA BIBLIA, ambacho ni mpango wa kusoma sura tatu kwa kila siku moja, na kitakuchukua kusoma Biblia kwa mwake mzima (Agano Jipya mara mbili). Endelea kusoma Biblia kila siku. Sio kitabu cha kusoma na kisha kukiweka chini. Kki kikisomwa tena na tena, Biblia itauvuta moyo wako, akili na maisha.
4. Je ungependa kukutana au kuandikiana na wa-Christadelphian popote walipo, au karibu na nchi yako? Unaweza kutaka kuwaandikia au, kama inafaa kufanya hivyo, kutana nao kwa ajili ya mazungumzo zaidi. Ikiwa wapo karibu kiasi cha kutosha unaweza kuhudhuria mikutano yao?
5. Unapenda kusoma zaidi juu ya mambo ya Biblia? Kama ndiyo, tafadhali mwandikie Mfunzi wako ni mambo yapi unayo vutiwa sana, Tuna vitabu vya maana sana vingi juu ya mambo ya Biblia.
6. Kama unaona unaweza kubatizwa jione kwamba unahitaji muda zaidi wa mafunzo, zipo kozi zingine zinazo patikana. Muulize Mfunzi wako.
7. Ikiwa unakubaliana na mambo yote yaliyo ndani ya Kozi hii ya kuandikiana, na unafikiria kuhusu kubatizwa, tafadhali tujulishe.

Nitabatizwa jinsi gani?

Kama ulivyo jifunza katika Somo la 31, ni muhimu uielewe injili, jinsi isivyo mchezo kubatizwa, na matokeo yatakayo kuwepo katika maisha yako. Ni jukumu letu kuhakikisha kuwa unafahamu kabla ya kukusaidia ili ubatizwe.

Hivyo uttakutumia maswali kadhaa ya kujibu - maswali yanayo husu mafundisho ya lazima ya Biblia na kuhusu mwelekeo mwingine wa vitendo vya kuishi maisha ya Kikristo. Baada ya hili, kama umejibu vema tutampanga mtu mmoja au zaidi katika washirika wetu wa Misheni kukutembelea.

Kama kweli upo tayari kwa ubatizo, jambo hili litapangwa popote panapo faa na pana maji ya kutosha.

Iwapo kuna kundi la wa-Christadelphia walio karibu utakuwa mshirika wa ikelezia hilo. Kama sivyo, basi tuta hakikisha kwamba unapokea mambo yaliyo chapishwa daima ya kukusaidia kusoma, na pamoja na vitabu vya kuwapa marafiki. Pia tutakutumia "maonyano" (yaani mambo ya kukutia moyo) - karatasi zinazo faa kwa ajili yako kwa kila juma Kuumega Mkate (ushirika) utumishi katika nyumba yako mwenyewe.

Kuhusu mimi vipi?

Maana ya kweli huja hapo tunapo anza kuelewa kwamba sisi ni wenye dhambi dhidi ya Mungu na kwamba Mungu pekee, kwa njia ya Yesu, aweza kutusaidia:

> *"Kwa maana wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu" (Rum. 3:23)*
>
> *"Bali Mungu aonyesha pendo lake kwetu, katika hilo, tulipokuwa TUNGALI wenye dhambi, Yesu alikufa kwa ajili yetu" (Rumi 5:8).*

"Hatua ya pili" kwa ajili yako inategemea kiasi gani ulicho badilika na kuchochewa na kile ulicho jifunza toka Neno la Mungu. Kila mmoja wetu yupo kwenye njia ya kutafuta wokovu tunapo anza kujifunza ukweli kuhusu sisi wenyewe; kama Yeremia aliposema:

> *"Ee Bwana, ninajua kwamba njia ya mwanadamu haipo katika nafsi yake; haipo ndani ya mwanadamu kuongoza hatua zake" (Yeremia 10:23).*

Je **una** ona kama hivyo? Je Mungu anaanza kukusisitiza kufanya kitu kingine kinacho husu "kuutafuta Ufalme wa Mungu na haki yake"?

Punde kidogo au baadaye, kila Mkristo inabidi aone haja ya kufanya mabadiliko katika maisha yake - badiliko la kuendelea kuwa mwenye dhambi au utoke ndani ya adamu, (yaani kutoka kuangamia jumla) na kuja kuwa mtakatifu "katika Kristo" (yaani, kuwa na tumaini la ufufuo Yesu akirudi na la uzima wa milele katika Ufalme wake).
Watu kidogo kule Yerusalemu, wakati walipo anza kuielewa kweli,

> *"walichomwa mioyo yao, na wakasema ... waume ndugu zetu, tufanyeje?"*

Jibu la mtume lilikuwa:

> *"Tubuni, na mbatizwe kila mmoja wenu kwa jina la Yesu kwa ondoleo la dhambi..." (Matendo 2:37,38).*

Ni tumaini letu kwamba umekuwa ukifikiria kwa makini sana kuhusu nafasi (maono) yako. Kwa maana hii huenda umekuwa na shaka kidogo. Hutaki mtu yeyote akusonge. Unataka muda wa kufikiria. Tunafahamu hilo!

Labda utapenda kuendelea kusoma na kujifunza Biblia kwa muda zaidi? Pengine ungependa kukutana na wa-Christadelphian wengine ili kuzungumia mambo? P Labda tayari umethibitishiwa kwamba unapaswa kubatizwa punde kidogo?

Kuabudu pamoja au mbali

Mfano wa waamini wa karne ya kwanza ndio wanao ufuata wa-Christadelphian hata sasa, na kila juma, hapo wanapo kuwepo washirika wanao ishi karibu, wanakutana ili kumwabudu Mungu. Mikusanyiko yao wanaiita "makelezia" (neno lililo na maana mkusanyiko wa watu wanao mwabudu Mungu) ili kuwakumbusha kwamba makanisa yanawahusu watu sio majengo. Wanakutana ili kufundishana Neno la Mungu, Biblia, kuhubiri injili (mikutano hii hasa hutolewa kwa wasio-washirika) na kila juma wanakutana ili kumkumbuka Yesu katika njia aliyo ipanga, kwa kushiriki mkate na divai katika utumishi wa Kuumega Mkate.

Kama waamini wa karne ya kwanza, hakuna makuhani au wachungaji ili kuongoza utumishi kwa sababu Bwana Yesu ndiye Kuhani wetu Mkuu. Watu wanao amini wanashiriki kazi ya kuhudumia. Mwanaume mmoja anasimamia - anapanga nyimbo za sifa na kusoma na maombezi (sala) na anawaita wengine ili kusaidiana kazi hizi. Mmoja aweza kuwa alitayarisha mazungumzo mafupi ya kutiana moyo - kuonyana. Wakati mioyo ya wale walio hudhuria kwa kufaa wamejitayarisha kumkumbuka Yesu. mifano ya mkate na divai wanashiriki pamoja - kama Yesu alivyo fanya kwenye Chakula cha Mwisho zamani. (Soma Luka 22:14-30).

Kunapo kuwa hakuna waamini wengine wanao ishi karibu, ni muhimu vitu hivi vifanywe kama nafasi inaruhusu. Wakati wa kuwafundisha watoto na watu wazima kuhusu injili utafika katika familia, au katika hali ya mambo mwengine. Kusoma Biblia na kuomba itakuwa ni kazi ya kila siku, na Jumapili itakuwa ni siku ya kumkumbuka Bwana kwa mkate na divai, kwenye utumishi wa kuumega mkate mtu peke yake, katika ushirika na wa-Christadelphian wote ambao wanafanya kitu kile kile ulimwenguni pote. Kwa muda, ambao unaweza kumpendeza Mungu kuwaita waamini wengine katika eneo hilo na hivyo ni kuruhusu maendeleo ya ikelezia jipya la wanao abudu.

Muhutasari

1. Ushirika wa Mkristo au Biblia ni kushiriki imani, matumaini na kuabudu pamoja na wale wanao amini na kutumaini mambo mamoja, na wanao mwabudu Mungu kwa usahihi, Maandiko, desturi.
2. Ushirika wa Biblia ni kuwa tofauti na wale ambao hawashiriki imani yetu.
3. Kwa sababu sio vema mwanamke au mwanaume kuwa peke yake, tutatafuta ushirika na ndugu-waamini mara kwa mara inapowezekana.
4. Yatupasa siku zote kutafuta ushirika pamoja na Mungu na Bwana Yesu kwa kupita kwenye sala, kutafakari na kusoma Biblia.
5. Ushirika ulio karibu kabisa na Mungu, Bwana Yesu na ndugu zetu waamini ni wakati tunapo shiriki mkate na divai katika utumishi wa Kuumega Mkate.
6. Kutakuwa na ushirika kamili na Mungu katika Ufalme wake duniani.

Sura za kusoma: 1 Yohana 1; Warumi 14-15:7; 1 Wakorintho 10
Jifunze kwa moyo: 2 Wakorintho 6:16

"Pana mapatano gani kati ya Mungu na sanamu? kwa maana ninyi ni hekalu la Mungu aliye hai; kama Mungu aliposema, nitakaa kati yao, nitatembea pamoja nao; nami nitakuwa Mungu wao, nao watakuwa watu wangu. "

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na39.

MUHUTASARI WA MAFUNZO YA BIBLIA

1. **Injili**
   Hii ni Habari Njema ya Ufalme wa Mungu utakao wekwa duniani Ujumbe huu unapatikana katika Agano la Kale na Agano Jipya.
   Mwanzo 22:17, 18
   Mathayo 4:23
2. **Biblia ni Neno la Mungu**
   Waandishi 40 wa vitabu 66 waliongozwa na Mungu.
   Zaburi 68:11
   2 Petro 1:21
3. **Mungu ndiye aliye umba ulimwengu**
   Kila kitu duniani kiliumbwa kwa ajili ya faida ya wanadamu, pamoja na kusudi kwamba dunia ijae na utukufu Wake. Yesu Kristo ndiye kitivu cha shabaha yake.
   Mwanzo 1:1
   Hesabu 14:21
   Zaburi 103:8-11
   Isaya 45:18
4. **Yesu atarudi tena duniani**
   Alikuja karibu miaka 2000 iliyopita kuhubiri na kutoa uhai wake kama "Mwana Kondoo aliyeechinjwa tangu kuwekwa msingi wa ulimwengu". Kwa sasa yupo mbinguni, lakini atarudi kama mfalme wa dunia.
   Mathayo 25:31-34
   Matendo 1:10-11
   Matendo 3:20,21
   Ufunuo 22:20
5 **Kurudi kwa Yesu kumekaribia sana**
   Unabii umetimia na kuna ishara nyingi leo zinazo onyesha kwamba ujaji wake umekaribia. Kwa mfano: Wayahudi na Taifa la Israeli; maasi; vitisho; njaa; misiba mikubwa na matetemeko ya ardhi.
   Luka 21:10-11
   Luka 21:24-33
   2 Timotheo 3:1-5
6. **Ufalme wa Mungu utakuwa duniani**
   Huu ni kitovu cha ujumbe wa Biblia. Ufalme tunao uomba katika sala ya Bwana makao yake makuu yatakuwa Yerusalemu nchini Israeli, ambako Yesu atatawala miaka 1000 juu ya mataifa yote kwa amini. Baada ya hapo, hapatakuwa na dhambi wala mauti tena.
   Isaya 25:23
   Yeremia 3:17
   Mika 4:1-8
   Ufunuo 11:15
7. **Mungu alimwahidi Abrahamu**
   Abrahamu, kwa sababu ya utii wa uaminifu kwa Mungu, aliahidiwa kwamba yeye na familia yake (Wayahudi) wataimiliki nchi ya Israeli na kwamba mmoja wa mzao wake (Yesu) atakuwa mfalme wa ulimwengu.
   Mwanzo 12:1-3
   Mwanzo 15:5-6
   Mwanzo 22:15-18
   Galatia 3:8, 16, 29
8 **Wayahudi ni watu wa Mungu**
   Walikuwa wawe ni mashahidi wa uwepo wa Mungu na nguvu. Bali waliasi na wakatawanywa duniani pote. Biblia ilitabiri kuwa "siku za mwisho" watarudi katika nchi ya Israeli.
   Isaya 11:11,12
   Isaya 44:8
   Ezekieli 37:21, 22
   Warumi 9:3-5

Lakini mambo haya hakutoshi **kuyajua** kwenyewe.

Hata hivi, wanaume wengi na wanawake wanakwenda kwenye vyuo ili kujifunza dini na kupata vyeti au kupata kazi ya "utumishi". Lakini hiyo haiwageuzi (hawaongoki) na kuwa Wakristo. Wale Christadelphian Bible Mission haitoi digrii au vyeti vya elimu ya kujua Biblia.

Tunaihubiri injili kwa sababu tunajua kwamba Mungu anapenda kuongeza neema yake kwa njia ya Yesu, kwa wote wanao taka kuokolewa toka dhambi zao. Mungu anamwalika kila mwanaume au mwanamke anaye kubali njia yake ya wokovu ili kushiriki kwenye Ufalme wake.

Inamaanisha kitu gani kuwa Mkristo

Wakristo wa kweli ni watu wanao amini amri za Yesu na walio chagua ili wabatizwe na kuishi kama wafuasi wake, wenyewe wakiwa tayari katika utumishi pamoja na Bwana hapo atakapo rudi kama Mfalme wa ulimwengu.

Wakristo wa kweli wapo tofauti toka watu wengine wote, kwa sababu wameitwa na wajifunze kwa ajili ya Ufalme unao kuja duniani. Muumba ana mpango mmoja tu kwa ajili ya dunia na jinsi tunavyo itikia mwaliko wake ili kuja kushiriki katika mpango huo yatupasa kuwa wamoja popote tunapo ishi.

Mungu hana mikondo ya amri kwa ajili ya wanaume na wanawake walio India, na mkondo mwingine kwa wale walio Uarabuni, au Afrika, au Karibiani, au Visiwa vya Pasifiki. Kuna mwokozi mmoja tu, na njia moja ya kuweza kuokolewa. Kama mtume Petro aliposema:

> *"Wale hakuna wokovu kwa kupitia mwingine yeyote: kwa maana hakuna jina lingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu, liwapasalo kuokolewa kwalo" (Matendo ya Mitume 4:12).*

Kwa nini kuna makanisa mengi?

Unaweza kuuliza: "Basi, kwa nini kuna madhehebu mengi mno na makanisa tofauti?"
Hilo ni swali ambalo lina wapa wasi wasi watu wengi wanao fikiria kujiunga na jumuia ya Kikristo.
Lakini fikiria ukweli huu: sio Mungu aliye yagawa makanisa ya watu Wakristo katika "Katholiki", "Waporestanti" au "Wapentekosti". Jibu ni kwamba katika mambo mengi ilikuwa ni watu waliopenda umaarufu "ambao waliwaongoza wafuasi wao wawafuate" ili kwamba watengeneze vikundi. Wengi walikuwa ni wenye "busara" pia kusikiliza injili iliyo hubiriwa na Yesu na wafuasi wake. Walifanya kile Mtume Paulo alicho tabiri:

> *"Maana utakuja wakati watakapo yakataa mafundisho yenye uzima ili kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo ya kweli, watazigeukia hadithi za uongo" (2 Timotheo 4:3,4).*

Je utaitikia mwito huu?

Mstari wa mwisho wa kujifunza: Matendo ya Mitume 17:30-31

"Basi, zamani zilikuwa za ujinga Mungu alijifanya hazioni; basi sasa anaagiza watu wote watubu kila mahali. Kwa maana Mungu amepanga siku atakayo hukumu ulimwengu kwa haki kwa mtu yule aliye mchagua; kwani ameweka uthabiti mambo hayo kwa kumfufua toka wafu."

MASOMO YA BIBLIA KWA NJIA YA POSTA YA WAKRISTADELPHIAN Na40.

HATUA YA PILI

Soma: Matendo ya Mitume 2

Imekuwa ni furaha yetu kubwa kushirikiana nawe katika Kujifunza kozi hii ya Biblia. Sasa tumefikia mwisho wa masomo haya na pengine utajiuliza: Baadaye ni kitu gani? Nifanye nini sasa?

Kabla ya kujaribu kutoa msaada mwingine pamoja na maswali haya ni jambo la muhimu kukumbuka Kozi hii inahusu kitu gani.

Tumekuwa tukikutambulisha mafundisho ya Biblia. Lakini ujumbe katika masomo haya haukuwa ni ujumbe **wetu** tu. Kila mara ulifungua na kusoma Biblia yako, ulikuwa unasikiliza toka **Neno la Mungu**. Hii ni njia ambayo Mungu anawafundisha wanaume na wanawake kuhusu Yeye mwenyewe na mpango alio nao kwa ulimwengu. Kwa sababu umeliangalia Neno la Mungu. alikuwa anazungumza **nawe** na kutumainia jibu toka **kwako**.

Biblia yote ni uongozi wa Mungu na ina nguvu kubwa ya kuweza kuyabadili maisha yako. Ikiwa katika kukuhubiria injili kwa kupitia karatasi hizi, tumeweza kukusaidia wewe kwa kukuvuta ili uyachuguze Maandiko wewe mwenyewe, basi tunafurahi sana.

Masomo yamekuvuta kwa jinsi gani?

Huenda umejifunza mambo mengine ambayo kabla hukuwahi kuyajua. Umewafikiria watu wakuu kama Abrahamu au Daudi. Umeona

- jinsi injili inavyopatikana katika Agano la Kale sawa sawa na Agano Jipya;
- jinsi Wayahudi ni mashahidi wa Mungu kati ya mataifa;
- jinsi Bwana Yesu alivyo ishi na kufa ili kuwaokowa wanaume na wanawake ambao wanamwamini;
- jinsi kifo na ufufuo wa Yesu vilivyo toa uhakikisho wa Mungu na mipango yake ijayo;
- namna Yesu atakavyo kuja duniani na kuusimamisha ufalme wa Mungu.

9. **Yerusalemu utakuwa ni kitovu cha dunia**
Yesu alikuwa ni Myahudi. Wazao wengi wa Wayahudi ambao wali msulubisha Yesu watampokea kama Masihi wao. Yerusalemu utakuwa makao makuu ya Ufalme wa Mungu na Israeli watakuwa "kichwa cha mataifa". Wasafiri toka kila nchi watazuru Yerusalemu kuabudu.
Yeremia 3:17
Mika 4:1,2
Zakaria 14:16
Mathayo 5:34-35

10. **Mungu alimwahidi Daudi**
Mfalme Daudi aliambiwa kuwa atakuwa na mtoto ambaye ataketi kwenye kiti chake cha enzi milele. Unabii huu ulimuhusu Yesu.
2 Samweli 7:12-16
Luka 1:30-33

11. **Yesu ni Mwana wa Mungu**
Alizaliwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu toka kwa mama yake Mariamu. Kwa njia hii yote mawili "Mwana wa Mungu" na "Mwana wa Adamu". Siku zote Yesu alisema kuwa Baba yake (Mungu) ni "mkuu kuliko mimi". Hakuna chochote kinacho dokeza kuwa Yesu alikuwa Mungu.
Mathayo 1:20-25
Yohana 14:28
Warumi 1:3,4
Wagalatia 4:4

12. **Yesu aliishi maisha yasiyo na dhambi**
Ingawa alikuwa ni mwanadamu, Yesu alikuwa ni Mwana wa Mungu na kwa hivyo aliweza kuyashinda majaribu yote na aliishi maisha makamilifu. Aliwawekea mfano wa kuishi wafuasi wake wote.
Isaya 53:5, 12
2 Wakorintho 5:21
1 Petro 2:22

13. **Yesu alikufa msalabani kwa ajili yetu**
Ilimpasa afe, kama watu wote, kwa sababu alikuwa ni uzao wa Adamu. Lakini kwa kuwa alikuwa hana dhambi akawa ni sadaka kamilifu ("Mwana Kondoo wa Mungu") kwa kifo chake. Kwa sababu hii anao uwezo wa kuonda dhambi zao wano kufa pamoja naye kwa njia ya ubatizo.
Yohana 1:29
Yohana 3:16
Wagalatia 1:4

14. **Yesu alifufuliwa kutoka kaburini**
Kwa sababu hakufanya dhambi "kaburi halikuweza kumshikilia". Mungu alikuwa na haki ya kumrudisha kwenye uhai tu mtu mwenye haki. Bwana Yesu Kristo alikuwa ni "limbuko" - uhaki ka kwamba wale walio katika Kristo watafufuka toka wafu aki rudi.
Matendo 2:24
Matendo 17:31
1 Wakorintho 15:22-23

15. **Roho Mtakatifu ni uweza wa Mungu**
Uweza wa Mungu upo dhahiri katika uumbaji wake. Wakati Mungu anapotumia Roho wake kwa makusudi maalum ameitwa "Roho Mtakatifu" Roho Mtakatifu hatendi peke yake toka kwa Mungu; hayupo katika hali ya upekee, bali ni uweza wa Mungu sana.
Isaya 61:1-3
Luka 1:35
Matendo 10:38
2 Petro 1:21

16. **Mshahara wa dhambi ni mauti**
Mauti ni adhabu kwa ajili ya dhambi kwa wanadamu. Tangu Adamu alipo asi hapo mwanzo, wote wametenda dhambi isipo kuwa Yesu na hivyo wote wamekufa. Wanaume na wanawake wote wataangamia kaburini ila wajue makusudi ya Mungu, na waiitikie injili.
Mwanza 3:17-19
Warumi 5:12
Warumi 6:23

17. **Zawadi ya Mungu ni uzima wa milele**

Hatuwezi kupata uzima wa milele. Bali, Mungu kwa upendo wake, ameahidi kuutoa uzima kwa wale wanao amini Neno lake kusadiki kwa Bwana Yesu na kujitahidi kufanya mapenzi yake.

Yohanna 17:1-3
Warumi 2:6-8
Warumi 5:15
Warumi 6:23

18. **Kutakuwa na ufufuo wa wafu**

Lakini sio kila mmoja atakaye fufuliwa. Yesu atawatoa kwenye makaburi wale ambao walikuwa na nafasi ya kuuitikia ujumbe wa injili ya wokovu,

Yohana 5:28,29
1 Wakorintho 15:12-19
2 Timotheo 4:1

19. **Kutakuwa na hukumu**

Wale ambao waliuelewa mwito wa injili yawapasa wasimame mbele ya Mfalme atakapo rudi duniani, aidha kuadhibiwa kwa mauti ya mwisho au kuzawadiwa uzima wa milele. Pia kuakuwa na hukumu kali kwa watu watakao mpinga Yesu atakapo rudi.

Danieli 12:1-2
Yohana 5:28-29
2 Wakorintho 5:10
2 Wathesalo. 1:7-9

20. **Kuishi milele**

Wale ambao watapewa uzima wa milele watakuwa na tuzo ya kumtumikia Bwana Yesu duniani na chini yake, watatawala watu watakao kuwa bado wanakufa. Hatimae wanao kufa wata kufa na watafufuliwa tena baada ya miaka 1000 kuisha; lakini "watakatifu" watafurahia afya kamili na furaha wakati wakihubiri "injili ya milele" na kuifanya dunia ni mahali pa ajabu kuishi.

Zaburi 37:9-11, 22
Danieli 7:27
Ufunuo 20:4-7

21. **Malaika ni wajumbe wa Mungu**

Mungu aliwaumba malaika kuwa watumishi wake milele. Hawafi kamwe na wanatimiza mashauri ya Mungu katika ulimwengu. Na pia wanawaangalia wale walio duniani ambao wameitwa na Mungu kuwa "watakatifu" wake.

Kutoka 23:20-21
Zaburi 103:20
Waebrania 1:13, 14

22. **Ibilisi na Shetani**

Katika Biblia "ibilisi" ni nguvu ya dhambi iliyo ndani ya kila wanaume na wanawake wote. Wale wanao pinga mapenzi ya Mungu mara nyingine wameitwa "shetani". Hakuna katika Biblia malaika mwovu au mungu aliye nje ya mtu, ambaye anawajaribu ili wafanya dhambi.

Mathayo 16:23
Yohana 8:44
Matendo 10:38
Yakobo 1:13,14

23. **Yatupasa tutubu sisi sote**

Mungu anataka kuwa tutambue dhambi zetu, na kuzisikitikia na wakati unao kuja tujaribu kuishi kwa utofauti. Hatuwezi kutumaini wokovu ila tufanye hili. Toba maana yake maisha yote mapya, kumfuata Yesu.

Zaburi 51:1-10
Mathayo 4:17
Luka 13:1-5
Matendo 3:19

24. **Ubatizo wa mtu mzima katika**

Maji Hii ni lazima kabisa, lakini yatupasa kuelewa na kuamini mafundisho ya Biblia na amri za Yesu kabla ya kubatizwa. Ubatizo ni ishara ya kufa na Kristo kwa ajili ya dhambi zetu na kufufuka tena katika maisha mapya.

Mathayo 28:19-20
Marko 16:16
Matendo 2:38

25. **Wakristo hawapigani**

Mfuasi wa Kristo hatumii nguvu wala hajiungi na jeshi au Polisi Inampasa "Kuwapenda adui zake" kama vile rafiki zake.

Mathayo 26:52
Luka 6:27-29
Luka 22:25
Warumi 13:1,2

26. **Ndoa ya Kikristo**

Biblia ipo wazi kabisa kuwa Mungu alikusudia meme awe na mke mmoja, na wawili waitunze familia katika utauwa. Kulingana na shauri hili Mkristo asitake kuachana, wala kujiingiza katika mitara.

Mwanzo 2:21-24
Mathayo 19:3-6
Waebrania 13:4

27. **Wajibu wetu kwa Serikali**

Wakristo hutii sheria zote za nchi zao, isipokuwa zikipingana na sheria za Mungu. Kwa sababu uwenyeji wao ni kwenye Ufalme wa Mungu kwa hiyo hawana muda wa kujihusisha na siasa za uongozi wa ulimwengu. Tunaweza kujikuta tunapingana na Mungu.

Mathayo 22:21
Rumi 13:1-7
1 Petro 2:17

28. **Wakristo wanaweza kuomba ili wasamehewe dhambi zao.**

Hii ni moja ya tuzo ya kuwa "katika Kristo" (walio batizwa). Bwana Yesu yupo mbinguni, akitenda kazi ya ukuhani kwa ajili ya wafuasi wake na anamwomba Mungu asamehe uovu wao.

Wafilipi 4:6
1 Timotheo 2:5
Waebrania 7:24-26
1 Yohana 1:9

29. **Kusomo Biblia ni Muhimu**

Kusomo Biblia kila siku ni sawa na kula chakula kila siku. Mungu anazungumza nasi katika Neno lake. Twajifunza toka mifano ya Maandiko na kuna mafungu ya maneno yanayo faa kwa kila tatizo letu, na mahitaji.

Zaburi 119:89-112
Matendo 17:11-12
2 Timotheo 3:16, 17

30. **Ushirika pamoja na kifo cha Yesu**

Wakristo wanakumbuka kifo cha Yesu kwa "mkate na kunywa divai" kama Yesu alivyo agiza kwenye mlo wa mwisho. Kumbukumbu hii inajumuisha ahadi kwamba wafuasi wake watashiriki naye chakula kwenye Ufalme wa Mungu.

Marko 14:22-25
Luka 22:14-20
1 Wakorinth. 11:23-28

31. **Undugu wa kweli**

Hiki ni kitu kingine ambacho wanaweza kushiriki tu wale walio amini na wanajizoeza mafundisho mamoja ya Biblia kama yalivyo fundishwa wa Bwana na wafuasi wake karne ya kwanza. Wa-Christadelphian wana undugu wa ajabu pamoja na maelfu ya ndugu wa kiume na wakike nchi nyingi duniani.

Yohana 17:19-18
Matendo 2:41-42
Waebrania 10:24-25
1 Yohana 1:3-7

32. **Mwito wa Injili**

Mungu awaita watu wote kutoka mataifa yote, ili wamfuate Yesu na kij kujitayarisha na Ufalme unao kuja.

Mathayo 16:24-26
Matendo 15:14
1 Wakorintho 1:26-27
Wagalatia 3:27-29